**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**
**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Mkuu wa Shule 0759843430/0685784780**
**Makamu Mkuu wa Shule 0753225444/0786489450**
**Matron 0620176923/0757500686**

**SHULE YA SEKONDARI MANGA**
**S.L.P 305**
**TARIME-MARA**
**JUNE, 2024/2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

**YAH:MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MANGA HALMASHAURI YAWILAYA YA TARIME, MKOA WA MARA. MWAKA JULAI, 2024/2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka julai, 2024/2025 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Manga ipo umbali wa Kilometa 04 kutoka barabara kuu itokayo Mwanza kwenda Sirari.Wanafunzi wanaotoka mikoa jirani tofauti na mkoa wa Mara wa kifika Mwanza waende stendi ya Nyamhongoro wapande magari yaendayo Sirari washuke kituo kidogo kitwacho Gachuma/ Komaswa. Hapo wachukue pikipiki nauli ni Tsh. 2000/= hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza mwezi julai, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ............. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -**

**2.1. Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili rangi ya idara ya maji rinda box kitambaa kizito na iwe ndefu kufikia vigoko vya miguu**.** Ili kuepusha mkanganyiko wa rangi na mishono tofauti. Sketi zitapatikana shuleni kwa Tsh.25,000/= kwa kila sketi.
ii. Shati 02 nyeupe ya mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Sare ya Michezo ni Raba nyeupe, track suit ya light blue ikiwa na T-shirt yake.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
vi. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu.
vii. Track suit rangi ya Kijivu kwa ajili ya masomo ya usiku (prepation time)
viii. Sweta rangi ya dark blue (V-shaped) kwa mzazi anayependa kununua shuleni itapatikana kwa Tsh.20,000/= ikiwa na nembo ya shule.
ix. Nguo za kushindia /kuvaa wakati wa shughuli za nje ni magauni mawili rangi ya pinki rose mshono wa solo ndefu hadi chini. Kwa mzazi anayependa kununua shuleni itapatikana kwa Tsh.30,000/= kwa kila gauni.
x. Tisheti 02 rangi ya dark blue yenye kola ya "cream". Kwa mzazi anayependa kununua shuleni zitapatikana kwenye duka la shule kwa Tsh.15,000/= kwa kila tisheti ikiwa na nembo ya shule.

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari, Kaunta book nane na kalamu za kutosha rula moja na mathematical set.
ii. **Ream 02 (Double A)** kwa mwaka.
iii. Vitabu vya masomo kwa tahasusi husika (Combination) mfano kwa shule hii ni **CBG**, **PCB, HGK** na **HGL**

| S/N | SOMO | AINA YA KITABU |
|---|---|---|
| 1. | BIOLOGY | 1. New Understanding Biology For Advanced Level By Suzane Toole, Complete Advance Biology By Respicius R.<br>2. Biological by Taylor DJ, Adv. Manual |
| 2. | CHEMISTRY | 1. A. Level chemistry By EN. RAMSDEN<br>2. A-level Physical chemistry 6*th* Edition by HEYS<br>3. Advanced chemistry review by William W. Davies By MZUMBE BOOK PROJECT |
| 3 | GEOGRAPHY | 1. An intergrated approach by Waugh D.2009. Geography landscape appreciation By Mack night<br>2. Practical Geography for Africa By S.M Pritchand<br>3. Practical Geography A-level by KAMILI Z.2011 |
| 4. | PHYSICS | 1. Principle of Physics class xi and xii By S .CHAND<br>2. A-level physics By ROGER MUNCASTER |
| 5. | HISTORY | |

| | | |
|---|---|---|
| | | 1. Essential in Advanced level History – paper 1 by SALEHE YASIN<br>2. Essential in Advanced level History – paper 2 by SALEHE YASIN |
| 6. | KISWAHILI | 1. Fonolojiaya Kiswahili sanifu (FOKISA) sekondarinavyuoBy MASSAMBA DPB na WENZAKE<br>2. Fasihiya Kiswahili, Chuo kikuuHuria cha Tanzania By MULOKOZI, MM 1996 |
| 7. | ENGLISH LANGUAGE | 1. The Real English Text Book For Advanced Level Form 5 & 6 By KADEGHE MICHAEL, 2010<br>2. Advanced English language, Form 5 & 6 By DSM OXFORD UNIVERSITY PRESS, 2012. |
| 8. | GENERAL STUDIES | 1. Understanding Advanced level General studies By JAMES BIGIRAMUNGU & SM. DEOGRATIAS 2012 |

**MUHIMU:** Mzazi/mlezi unashauriwa umnunulie mwanao vitabu vilivyoorodheshwa kulingana na tahasusi aliyochaguliwa kwani vitabu hivyo vitakaguliwa siku ya kuripoti shuleni.

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma somo la Biology;
v. Scientific Calculator fx991
vi. Godoro la futi tatu.
vii. Mashuka Shuka pea mbili, pea moja ya light blue na pea moja ya pink na foronya zake Jozi 2, blanket 1, chandarua 1
viii. Nguo za ndani za kutosha; tauro moja, kanga pea moja ya kuogea ,pedi pakti 06 na night dress.
ix. File moja la kutunzia kumbukumbu zake ofisini (aina ya spring file) ambalo itapatikana kwenye duka la shule kwa Tsh.2000/= kwa mzazi atakayependa kununua shuleni.
x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xi. Ndoo 2 ( ndogo lita Kumi1 na kubwa lita ishirini 1) zenye mifuniko;
xii. Kiwi, dawa ya meno, mswaki na brush.
xiii. Dawa ya chooni lita 5 aina ya dexi inapatikana kwenye duka la shule kwa Tsh. 10,000/=. Kwa mzazi atakayependa kununua shuleni.
xiv. Dawa ya mbu (HIT) kubwa
xv. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
xvi. Aje na nakala ya result slip
xvii. Kama ni mgonjwa aje na cheti cha Daktari.

## VIFAA VYA USAFI

| TAHASUSI | VIFAA ATAKAVYOLETA |
|---|---|
| PCB | Fyekeo,jembe na mpini, dawa ya chooni aina ya dexi, soft broom 01 na Squizer. |
| CBG | Squizer,jembe na mpini,reki na dawa ya chooni aina ya dexi,soft broom 01 |
| HGK | Fyekeo, jembe na mpini, mfagio wa nje 01, dawa ya chooni aina ya dexi , hard broom 01 na reki. |
| HGL | Fyekeo,jembe na mpini, reki, dawa ya chooni aina ya dexi, soft broom 01 na Squizer. |

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

3 Michango hii iliyoorodheshwa hapo juu ilipwe kwenye akaunti namba **30401200103 NMB BANK** jina la akaunti **MANGA SECONDARY SCHOOL**. Mwanafunzi aje na pay in slip na wakati wa kulipa yaandikwe majina kamili ya mwanafunzi.

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayonipamojana;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kuhama bweni.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum kutoka kwa Mkuu wa Shule ikiwa kama ni mgonjwa au kwa sababu za msiba.**
- **BIMA YA AFYA. mwanafunzi aje na bima yake ya afya kwa matumizi yake. Ili kuepusha gharama za matibabu.**

### 3.2 Makosa yatakayo sababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi isiyoruhusiwa katika mazingira ya shule na nje ya mazingira ya shule kipindi akiwa shuleni bila

kibali maalumu. Faini Tsh.100,000/= ili kamati ya nidhamu iweze kumjadili mwanao.

xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wakaribu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu ili mwanao aweze kupata elimu bora.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MANGA**

Wako,



**EDITHA L. NAKEI**
**MKUU WA SHULE**

HEADMISTRESS
MANGA SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 305
TARIME.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **mkuu wa shule ;- 0759843430/0685784780**

- **makamu mkuu wa shule ;- 0753225444/0786489450**
    - **mwandamizitaaluma ;-  0759752032**

## OFISI YA RAIS-TAMISEMI
## SHULE YA SEKONDARI MANGA
## HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI

1. JINA LA UKOO……………………………………………….JINA LA KWANZA…………………………………………………..
   JINA LA KATI…………………………………………………………….
2. JINA LA MZAZI / MLEZI………………………………………………………………………………………………………
3. KAMA NI MLEZI: UHUSIANO………………………………………………..NAMBA YA SIMU……………………………
4. ANUANI YA KUDUMU YA MZAZI/MLEZI…………………………………………………..
5. TAREHE YA KUZALIWA ……………………………………………..
6. MAHALI MWANAFUNZI ALIPOZALIWA:- KIJIJI CHA ……………………………KATA YA……………………………..
   WALAYA YA ………………………………MKOA WA …………………………………..
7. DINI…………………………………………………………….DHEHEBU……………………………………………..
8. UNAINGIA KIDATO CHA ……………………………….TAREHE /MWAKA………………………………………
9. KUTOKA SHULE YA MSINGI…………………………WILAYA YA …………………………MKOA WA ………………
10. MZAZI/MLEZI WAKO ANAFANYA KAZI YA AJIRA/MKULIMA/BIASHARA……………………………………….
11. NDUGU WENGINE AMBAO WANAWEZA KUPELEKEWA HABARI NUHIMU JUU YAKO.
    i. JINA………………………………………………….UHUSIANO…………………….NO. SIMU……………………..
    ii. JINA………………………………………………….UHUSIANO……………………..NO.SIMU……………………..
    iii. JINA…………………………………………………..UHUSIANO……………………..NO.SIMU……………………..
12. SIFA MAALUMU KAMA UNAZO……………………………………………………………………………………………
13. TAARIFA ZA WAZAZI:-
    i. WAPO WOTE……………………………………………………………
    ii. YUPO MMOJA (TAJA- BABA/MAMA)………………………….
    iii. WOTE WAMEFARIKI…………………………………….(Weka alamayavema (√)panapohitajika)

Nakirikuwamaelezoyaliyopohapojuunisahihi.

**……………………………………………………….** **……………………………………**

**SAHIHI YA MWANAFUNZI** **SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi (Jina la mwanafunzi)………………………………………………………………………nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga katika shule hii. Na ahidi kufuata sheria za shule na taratibu zote zilizotolewa na zitakazotolewa na uongozi wa shule.

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi (jina kamili) ………………………………………………………………………ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………………………nimeyasoma masharti na sheria za shule ya sekondari MANGA ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia mwema wataifa letu.

**TAREHE……………………………………………………………………** **TAREHE…………………………………………………………..**
**SAINI YA MWANAFUNZI……………………………………….** **SAINI YA MZAZI/MLEZI…………………………………..**
**JINA LA MWANAFUNZI……………………………………..** **JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………….**

## TARIME DISTRICT COUNCIL

MANGA SEKONDARY SCHOOL
P.O.BOX 305
TARIME
DATE:.............................

TO MEDICAL OFFICER
.......................................................
........................................................
.........................................................
Ref:................................................................................................................................(name of student)
Please examine the above named student as per medical examination form.

HEADMISTRESS

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by Government medical officer)

Full name................................................................................................................................
Age .................................................Height...........................................(Cm) Weight.......................(Kg)

1. Blood examination..........................................................................................................
2. Stool examination............................................................................................................
3. Urinalysis (Pregnancy) for female..................................................................................
4. Tuberculosis Test (TB) & Leprosy test.........................................................................
5. Eye......................................................................................................................................
6. Ear test .............................................................................................................................
7. Chest...................................................................................................................................
8. Abdomen............................................................................................................................
9. Asthma...............................................................................................................................
10. Spleen...............................................................................................................................
11. Any chronic complains noted above.............................................................................

Any addition information:
E.g.physical defects or impairments,chronics or family diseases like sickle sell, Inabilty to eat certain food e.t.c...........................................................................................................................................
I have examined the named above and consider that he/ she is physically FIT /NOT FIT to pursue secondary education.

............................................................ ...............................................
Signature and Officer Stamp Date
Station ...................................... Designation.............................